# DHANA LA FAMILIA YA KISALVATORIANI: WAZO LA BAADAYE

**Fr. Scott Jones SDS**

**1 June 2015.**

## Utangulizi

Mwaka 2007 ndio lilitokea tukio kubwa na la muhimu katika historia ya familia ya kisalvatoriani wakati hati ya familia ya kisalvatoriani ulipokubalika na uongozi wa juu wa kimataifa wa vikundi vitatu vya familia ya kisalvatoriani. (Baadaye hii hati ilipewa idhini oktober 2012). Kupewa idhini kwa hati hii ya familia ya kisalvatoriani ilikuwa ndyo hitimisho la mjadala mrefu wa kurudia kwenye charisima yetu ya mwanzo ya mwanzilishi wetu kupitia kwa mtaguso wa pili wa vatikano. Lakini makubaliano hayo yalisababisha mwanzo mpya kwa kutupa changamoto na hivyo kujiuliza, ni nini kitakachofuata baadaye.

Katika mfululizo wa makala hii na nyinginezo, mwandishi ataeleza kwa kifupi nia ya padre Jordan na hatua zilizofuata baada ya mtaguso wa pili wa vatikano kuwaingiza wanachama walei wa familia ya kisalvatoriani na kuwa na ushirikiano wa karibu kati ya haya matawi matatu ya familia ya kisavatoriani. (***Annales Vol xvi***) nitapendekeza maswali mawili ya kutilia maanani. Swali la kwanza, ***USHIRIKIANO WETU UTAKUWA WA NAMNA GANI HUKO MBELENI? Na la pili, KUTAKUWA NA FAIDA GANI TUTAKAPOJITAHIDI KUTAMBULIKANA KIMATAIFA KATIKA FAMAILIA YA KISALVATORIANI?*** Kwa sababu ya ufupi wa Makala hii, njia Mbadala zitapendekezwa ambazo zinaweza kutupa tafakari jinsi ya kufaidika tunapokuwa tunashirikiana kwa pamoja kama familia ya kisalvatoriani

## MAONO YA MWANZO YA PADRI JORDAN

Kazi nyingi ya wasalvatoriani imeelezwa na padri Yohane mbatizaji(baadaye ndio Maria wa msalaba). Nia ya padri jordan ilikua kuanzisha shirika la kitume la kufundisha (**APOSTOLIC TEACHING SOCIETY**), ambalo lingekuwa na muungano wa mapadri na walei ambao watashirikiana kwa kufanya kazi kwa ajili ya ufalme wa mbinguni. Shirika hilo, lingekuwa na matawi matatu. Sehemu ya kwanza itakuwa ni mapadri pamoja na walei ambao mwanzoni walikuwa wamesahaulika au kuachwa nyuma. Mfano kuwa na roho kama ya mitume wa kwanza waliokuwa wanafanya kazi kwa ushirika, na kwa kufanya kazi nyingi za kitume.( mwanzoni walikuwa na kiwanda cha kupiga chapa na umisionari wa kufundisha katika elimu). Kundi la pili, lilikuwa la wafanyikazi katika ofisi za kuchapa na kufundisha (yaani waandishi wa habari). Na kundi la mwisho lilikuwa la watu wote wanaofanya kazi ili waweze kusaidia shirika liweze kuendelea.

***"charisma ya familia ya kisalvatoriani ni zawadi ya roho aliyopatiwa padre jordan kwa ajili ya kanisa. Hii tunaiona kutoka mwanzo wakati shirika likianzishwa na padri Jordan mwenyewe december 8 , 1881 huko Roma. Mapadri wa jimbo ndio walikuwa wamachama wa kwanza kujiunga na shirika. Therese von Wuellenweber (baadaye mwenye heri Maria wa mitume)alijuinga na shirika mwaka 1882, baadaye walei wengine wengi walijiunga na shirika hili." HATI #2***

Bila shaka Jordani alikuwa mdogo sana, mdhanifu ambaye wakati huo alikuwa ni padri wa jimbo na mwanzoni alikuwa na uelewa mdogo wa muundo wa sheria za kanisa na jinsi ya kuzifanyia kazi. Machi 1883 ndio ulikuwa wakati muhimu, kipindi hiki, jordan aliweka nadhiri zake za utawa na akapewa vazi la utawa na pia jina jipya la utawa. Mwaka 1885 Oktoba ilikuwa kipindi kigumu katika maisha yake kwani kipindi hiki baadhi ya masisita walijitoa katika shirika lake na kujiunga na shirika la Mama wa mateso. ( hili ni tawi la

masista lililoanzishwa baadaye mwaka 1888 kwa kushirikiana na Therese von wullenweber, (baadaye ndiye Mama Maria wa mitume).

Mabadiliko ya haraka kutoka kwa shirika lenye hatua tatu hadi mashirika mawili ( mapadri na masista) ilimpa hamasa padre Jordan ile nia yake ya kwanza kufuatana na ukweli wa kanisa katika karne ya 19. Katika hatua hii ya mabadiliko , walei waliongezeka na walikuwa wanafanya kazi kwa umoja na ushirikiiano. Maisha yote yaliobaki ya jordan hadi kifo chake mwaka 1918, shirika la Mungu mwokozi na lile la masisita wa Mungu mwokozi walijikita katika kazi za kitume zaidi.

## KUANGALIA UPYA MAONO BAADA YA MTAGUZO WA PILI

Hati ya mtaguso wapili wa vatikano (***perfectae caritatis***) ( agizo la kurudia tena maisha ya kitawa) ilisisitiza mashirika ya maisha ya wakfu kuangalia upya charisma ya mwanzilishi wao. Kwa jumuiya na shirika hii ilifanya kuzama na kutafuta mwanzo wa **Shirika la Kitume la kufundisha,** kazi na mafundisho ya padri Jordan na yale ya Maria wa mitume. Kwa wasalvatoriani wengi hii ndio ilikuwa nia ya kwanza ya padri Jordan. Kutoka mwanzoni nia yake ilikuwa kuwe na ushirikiano kati ya wanajumuiya na shirika kwa jumla na pia kuwepo ushirikiano na walei pia. ( katika historia ya wasalvatorian mara nyingi hamna "walei" kati ya wasalvatoriani isipokuwa wanachama wengine ambao hawajapadrishwa yaani mabruda. Ila katika taasisi nyingi za kisalvatoriani kulikuwa bado kuna wafanyakazi ambao ni walei pia na wengine ndio wafhadili wa shirika. Lakini walikuwa hawakuwazingatiwa kama ni wasalvatoriani.

Pia ilikuwa ngumu kutia maanani nia ya kwanza ya Jordan katika Shirika la **Kitume la Kufundisha** lenye hatua tatu. Jaribo lolote la kufanya hivyo lilielekea kuvuruga maendeleo kwa wasalvatoriani. Lakini Marekani , mwanzo wa mkutanoo mkuu wa 14 mwaka 1970, walipendekeza uwezekano wa kuanzisha programu ya kuunganisha matawi hayo matatu utiliwe maanani. Mkurugenzi wa programu hii padre Ramon Wager aliteuliwa aone uwezekano wa kuanzishwa kwa program hii. Kwa muda wa miaka mitano, sio tu kwamba programu hii ilifaulu lakini pia katika mkutano mkuu wa 12 wa shirika katika provinsi ya Marekani kaskazini programu hii ilikubalikana kutiwa moyo kwa masharti ya kuwa na sheria za jumuiya au shirika la maisha ya utawa ili lisiweze kuwa matatani.

Kwa muda wa miaka mingi, shirika la kimataifa liliendelea kufanya kazi ambayo ilianzishwa na walei. Tangu lilipoanza marekani, programu zingine zilianzishwa katika sehemu nyingine, kwanza brazil na austria, halafu katika nchi zingine ambazo wasalvatoriani wanafanya kazi. Mkutano mkuu wa kumi na tatu ulielekeza kuwa makao makuu ya shirika lazima iwaelimishe wanashirika kuhusu mahusiano kati ya shirika na wale waliojiunga nasi kwa roho na kazi ya utume ya mwanziliishi.

Mkutano mkuu wa kumi na nne ambao ulifanyika mwala 1987 uliendelea kuunga mkono swala hilo. Na hii ilishababisha kuundwa kwa tume ya kimataifa ambayo ilikuwa na wawakilishi kutoka kwa kila tawi ili waweze kusoma na kujua uhusiano wa karibu kati ya chama na walei wasalvatoriani. Mkutano wa kwanza wa kimataifa uliofanyika huko Roma mwka 1990 , pia na wa pili uliofanyika San paulo Brazil mwaka 1992, ulisisitiza kuelewa kuhusu wito na charisma ya wasalvatoriani walei pamoja na ushirikiano wa karibu kati ya makundi haya matatu ambayo yalifahamika kama "FAMILIA YA KISALVATORIANI".

Mkutano mkuu wa 16 mwaka 1999 ulidhinisha kuwa na Katiba kwa walei wasalvatoriani na pia kuwa na kielelezo cha hati au nyaraka ya kimataifa ya familia ya kisalvatoriani. Ambao mwishoni wa hati ya familia ya kisalvatoriani, na ilidhinishwa na viongozi watatu mwaka 2007 na mwishowe ikakubaliwa na matawi haya yote matatu mwaka 2012.

***"Leo hii familia ya kisalvatoriani ina aina tatu, kuna shirika la mungu mwokozi, shirika la masisita wa Mungu mwokozi na jumuiya ya kimataifa ya Mungu mwokozi. Sisi zote tumeungana na usirikiano wa missioni kama ilivyooelezwa na mwanzilishi wetu, kuwa na familia moja ya mitume, wanaojitoa na wenye kutangaza kokote duniani wokovu uliopatikana kwa Yesu Kristo." HATI #3***

Hati ya kisalvatoriani yenyewe ni tukio muhimu la historia la kugundua nia ya mwanzo ya padre Jordan, kama siyo muundo wa Shirika lake. Katika ibara ya pili, hati hii inaeleza kuwa, " Familia ya kisalvatoriani ni muonyesho wa charisma, na pia ni zawadi ya Roho Mtakatifu aliyopewa padre Jordan kwa ajili ya kanisa. Mizizi yetu tunaifuatilia kihistoria katika **Shirika la Kitume la kufundisha** lililoanzishwa na padre Jordan Desemba 8 mwaka 1881 huko Roma.

Hati inaendelea kuelezea kuhusu lengo , maisha ya sala na pia ushirikiano katika familia ya kisalvatorinai na pia kuheshimu karisma ya haya matawi yote matatu. Hati ya familia ya kisalvatoriani inaonekana kama ndiyo hitimisho la kipindi muhimu katika katika historia ya umoja wa kisalvatoriani; kwa kurudi katika maono ya mwanzo aliyokuwa nayo padre Jordan.

## NINI KIFUATACHO?

Kama kupitishwa kwa hati ya Familia ya Kisalvatoriani ni mwisho wa kipindi kimoja katika historia ya kisalvatoriani, ikubaliwe kuwa ni pia mwanzo wa kipindi kingine kipya. Sura hii mpya itakuwa na nini ndani yake? Ni jinsi gani familia hii ya kisalvatoriani itaweza kuishi hii zawadi kutoka kwa padre Jordani, iliyogunduliwa upya hivi karibuni?

Katika ibara ya 14 ya Hati inaeleza kuwa " kama familia ya kisalvatoriani, tunatafuta kutoa ushahidi wazi kwa binadamu wote wa kiume na wa kike, kutoka tamaduni tofauti na asili tofauti wote tumeitwa kufanya kazi kwa pamoja katika utume.. Sura ya 17 inaita kila nchi/kizio, kuanzisha kundi la kitaifa la uhamasishaji, kutoka kila kundi la familia ya kisalvatoriani. Katika jamii zile ambazo tayari zimeanzisha ushirikiano wa makundi haya matatu, uzoefu unaonesha kuwa ushirikiano wenye tija unadai muda mwingi, kujitambua na kuheshimiana. Ni swala la kuhuzunisha katika historia ya wasalvatoriani na ile ya Kanisa, kwamba wanaume (tofauti na wanawake) wamekua katika nafasi za kutoa maamuzi, na wakreli (tofauti na walei) wamekua na sauti zaidi. Ili ushirikiano wa kweli utokee, historia hii lazima ikubaliwe, na historia hiyo itambuliwe, na hivyo hatua wazi zichukuliwe kwa ajili ya kusaidia mawasiliano wazi na namna mpya ya kutoa maamuzi, yenye lengo la kuleta upatano ifuatwe.

Nchini Marekani ulianzishwa Muundo, ambao ulifanywa kuwa kundi la pamoja la Uongozi (Joint Leadershi Group). Ukianzishwa mwaka 1991, Umoja huu unaundwa na wanachama watatu kutoka kila tawi la Familia ya kisalvatoriani, mfano, kwa upande wa Shirika la Mungu Mwokozi, na Masista wa Mungu Mwokozi, mkuu wa provinsi, makamu wa mkuu wa provinsi na mshauri mmoja kutoka kila tawi la familia ya kisalvatoriani. Ukiheshimiwa ulazima wa kila tawi kuwa na uongozi na maamuzi yake ya mambo ya ndani, hasa ya kiuongozi, Muungano huu wa uongozi unatoa maamuzi yanayohusu familia nzima ya kisalvatoriani. Kundi hili lina bajeti yake binafsi na inapowezekana, utume mpya unaanziashwa kw aushirikiano, ukitumia fedha kutoka katika mfuko wa Umoja huu wa Uongozi.. Mfano mzuri wa ushirikiano huu ni timu ya utume ya Jordan, ambayo ni timu ya utume wa kisalvatoriani katika jimbo la Tucson, Arizona, utume ambao unawapa malezi walei katika jimbo ambalo halina vyuo vya kikatoliki vya kuweza kutoa malezi ya utume wa walei. Wanachama wanzilishi ni pamoja na padre mmoja , sista mmoja pamoja Msalvatoriani mlei.

Wakati kila tawi katika familia ya kisalvatoriani wanakuwa na utume wao wenyewe, kama hati ya familia ya kisalvatoriani inatakiwa iwe na maana, ni muhimu kila utume mpya ukaguliwe kama kuna uwezekano wa ushirikiano na kama inawezekana utume huo mpya uundwe kwa ushirikiano katika sehemu mbali mbali ya dunia. Utamaduni wa mahali unatakiwa uangaliwe kwa makini sana, na kwa msaada wa makundi ya kiuongozi ya kimataifa na kwa hekima wanayopata kutoka katika mikutano ya kimataifa, pamoja na uzoefu wanaopata wanapokuwa na mikutano ya kimataifa, njia mpya za ushirikiano zitasaidia muundo wa Kisalvatoriani wa Mtaguso Mkuu wa pili wa Vatikano, kuonesha sura ya Kanisa la Karne ya Ishirini na moja.

Swala jingine, linalohusiana na hili, Ijapokuwa ni swala lenye utata, ni lile la kuendelea kudai kutambuliwa na Kanisa Kisheria kwa Familia ya Kisalvatoriani. Kwa sasa Shirika la Mungu Mwokozi, na Masista wa Mungu Mwokozi, ni Mashirika ya kipapa ya maisha Wakfu, na Jumuiya ya Kimataifa ya Mungu Mwokozi inafuatilia kutambulika na Kanisa kisheria kama Umoja wa waumini, kupitia Kamati ya Kipapa ya walei. Hata kama Jumuiya ya Kimataifa ya Mungu Mwokozi ikikubalika na Kanisa kisheria, ukweli unabaki kwamba Maana ya kisheria ya Kanuni ya Familia ya Kisalvatoriani, haiwezi kuwa nyingine, isipokua ile ambayo inatolewa na matawi matatu ya familia ya Kisalvatoriani.

Kuendelea kutafuta Utambulisho wa kisheria ya kanisa kwa jili ya Familia ya Kisalvatoriani, kunahitaji juhudi endelevu, tafakari ya kina na kazi, lakini kwa maoni ya mwandishi wa makala haya, juhudi hizo ni muhimu sana kwa siku zijazo. Vizio vya zamani huko America kaskazini na Ulaya wanafanya kazi katika hali ya kupungua sana idadi, kwa miaka sasa, na vizio vipya wanafanya kazi, wakati mwingine katika mazingira ambayo, hadhi ya kisheria inayotambuliwa na Kanisa ndiyo jia pekee katika tamaduni ambazo hazithamini sana usawa wa kijinsia, au muundo wa ushirikiano kati ya walei na wakleri. Kutambulikana kisheria kwa Muundo wa jumla wa Familia ya Kisalvatoriani, kutasaidia kuhakikisha utekelezaji wa kweli wa Kanuni ya Familia na kwa wakati huo huo, kupata heshima inayotakiwa kwa viongozi mahalia wa Kanisa.

Japokua kila familia ya kikanisa ina historia yake na sifa za pekee, lakini Jumuiya nyingi mpya zimejijenga katika misingi ya Muundo wa Ushirikiano. Opus Dei, Miles Jesu, na Legio of Christ (ikiwa ni pamoja na kundi saidizi lake la Regnum Christi) ni mifano mitatu hai. Hata mashirika ya zamani sana, yanatafuta sasa kutambuliwa kwa juhudi zao za kufanya kazi kwa ushirikiano kati ya matawi yake. Mmoja wa mifano inayofahamika ni Umoja wa Utume wa Kikatoliki wa mtakatifu Vincent Palloti (UAC), ulioanzishwa mwaka 1835 na Palloti. Ufafanuzi wa Umoja huo wa Kitume wa Palloti, unaelezwa na Palloti mwenyewe katika maneno yafuatayo: “Utume wa Kikatoliki, ni utume wa kiulimwengu, ambao ni kwa ajili ya makundi yote ya watu, unadai mtu kufanya kile ambacho lazima afanye, na anachoweza kufanya kwa ajili ya utukufu mkuu zaidi wa Mungu, kwa ajili ya wokovu wake mwenyewe na wokovu wa jirani yake.”[1]

VincentiPalloti alipoanzisha Shirika la Utume wa Kikatoliki ( mapadre na mabruder wapallotine), Shirika la Masista wa Utume wa Kikatoliki, na Masista wamissionari wa Utume wa Kikatoliki, vikundi vingine mbali mbali vilianzishwa. Wakitafuta kutambuliwa kisheria kwa “Familia ya Kipalloti”,, mwaka 2003, Halmashauri ya Kipapa ya Vatikano ya walei ilitangaza Umoja wa Kitume wa Kikatoliki, kuwa Ushirika wa wazi wa Waamini. Matokeo yake ni kwamba, kila padre, bruda, sista, au mlei mpallotini, ni mwanachama wa Shirika linalotambulika kisheria, linaloitwa Umoja wa Utume wa Kikatoliki.

[1] “UAC/SAC”, Mtandao wa dunia wa Wapallotini.

Ingekua faida kwa Familia ya kislvatoriani kufikiri namna inavyoeza vile vile kupata kutambuliwa kisheria. Japokua faida hasa ingekua ni kupata ulinzi wa kisheria, lakini faida kubwa ambayo ingetokana na muundo huo, ingekua Mfano ambao Shirika lingetoa kwa Kanisa la Ulimwengu. Miaka hamsini baada ya mtaguso mkuu wa pili wa Vatikano, Karisma za kushauriana na kushirikiana zimefanya hatua kubwa, hasa katika nyakati zetu za Papa Francisco. Lakini bado kuna mengi ya kufanya, ili kufanya hayo yawe hali halisi ya maisha katika maisha ya Kanisa duniani. Kama Familia ya Kisalvatoriani itapewa nafasi kubwa, kutambulika kisheria kungesaidia sana kutoa Kinga ya Kikanisa na kutoa mchango mkubwa katika kupunguza u-kleri na u-jinsia katika Kanisa.

## HITIMISHO

Familia ya kisalvatoriani ina matukio mengi muhimu ya kihistoria; Mwaka 1881 lilianzishwa shirika la Kikatoliki la kufundisha (APOSTOLIC TEACHING SOCIETY), mwaka 1883 ilibadilishwa likawa taasisi ya maisha ya kitawa na mwaka 1888 ndio likawa shirika la kudumu la Mungu Mwokozi. Vizio vingine vipya navyo vina matukio yao ya muhumu ya kihistoria, kama uanzishwaji na ukuaji wake. Bila shaka kwa siku za usoni , mwaka 2007 na 2012 zitaadhimishwa kama tarehe muhimu za kihistoria, wakati Hati ya Familia ya Kisalvatoriani itakapopokelewa rasmi. Ni matukio gani mengine ya siku za usoni yatatambulika kama matukio muhimu ya kihistoria katika Familia ya Kisalvatoriani? Japokua majibu ya maswali hayo anayajua Mungu mwenyewe, ni wazi kwamba tarehe muhimu katika Familia ya Kisalvatoriani wakati ujao, zitategemea mwono mpya uliogunduliwa, kama alivyokua nao Padre Jordan mwenyewe. Tunaombea bidii zifanyike, ili wasalvatoriani wote wafanye kazi pamoja kudumisha na kufikia hizo tarehe mpya muhimu kwa faida ya Familia ya kisalvatoriani, lakini hasa kwa faida ya kukua kwa ufalme wa Mungu, ufalme ambao ni hasa wa ushirikiano, na uliojengwa katika usawa katika Ubatizo.

## MASWALI YA KUTAFAKALI

1 Soma tena hati ya familia ya kisalvatoriani kwa haya maswali ya kutafakali
   a) Andika au eleza maneno au sentensi inayokugusa na ujiulize: " Sentensi hii inaniambia nini, na ni jinsi gani naweza kuitikia?
   b) Familia ya kisalvatoriani inaweza kuwa na maana gani katika eneo lako la Dunia, na kwa ulimwengu mzima?
2. Baada ya kusoma makala haya, ungepewa nafasi ya kufanya marudio ya Hati ya Familia ya Kisalvatoriani, ungeongeza au kubadirisha nini?
3. Ni wapi unaona uzuri au ubaya wa familia ya kisalvatoriani kwa kutambulikana na vatikano?
4. Una ndoto na matazamio gani juu ya Familia ya Kisalvatoriani? Wewe kuwa mwanachama wa hii Familia, kunagusa namna gani maisha yako kama Msalvatoriani?